

Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA
KAZI YA KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE


JE, MMEPOKEA ROHO MTAKATIFU?

"Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" (Matendo 19:1-2a).

Wanafunzi wa Efeso walikuwa wameamini na kutubu lakini hawakujuu mpango kamili wa wokovu ambao wangeweza kupata kuitia kwa Yesu Kristo. Waliposikia injili walibatizwa. Baadaye ndipo Mtume Paulo aliwawekelea mikono, akawaombea, ndipo wakajazwa na Roho Mtakatifu.

Kuna watu wengi ambao washaomba ili kupata msamaha wa dhambi zao na wakampokea Kristo kama Mwokozi wao, lakini hawakuweza kupata maisha ya ushindi wa kiroho na utakatifu wake ambao huambatana na maisha hayo. Wao hukosa ujuzi wa kupata faraja ya kiroho. Wengi wao huanza kuishi maisha yao kwa ajili ya Bwana lakini muda si muda wao hujipata kwamba majaribu na mateso wanayopitia ni mengi sana hivi kwamba wanarudi kwa mambo yale ambayo Mungu aliwakomboa kutoka

nayo. Kwa wale ambao hawarudi tena katika maisha ya dhambi, maisha yao ya kiroho huwa ni ya kazi ya sulubu na wao huwa na utakatifu wa nje tu.



*"Mungu ataka
kukupatia kipawa cha
Roho Mtakatifu."*

Hebu tutazame maisha ya Mtume Petro. Kabla ya siku ya Pentekoste mtume huyo alisema kwamba alikuwa

amejitolea mhanga kwa Kristo, hivi kwamba akatoa upanga wake akiwa tarari kufanya vita kwa ajili ya Yesu wakati Bwana wake alipokamatwa katika Shamba la Gethsemane. Lakini muda si muda mtume huyo alimkana mara tatu tofauti na kusema kwamba hamjui Yesu. Wakati Petro alikumbana na majaribu na msukumo wa watu na hata kuona kwamba amechungulia mauti, yeye hakuwa na uwezo wa kuendelea kuwa mwaminifu. Lakini baada ya Roho Mtakatifu kushuka hapo katika siku ya Pentekoste Petro alihubiri ujumbe mpya kuhusu kufufuka kwa Bwana kwa nguvu na ujasiri mpya. Alikuwa sasa amejazwa nguvu na neema za Roho Mtakatifu ambazo ndizo humdumisha muumini. Kamwe hakurudi katika maisha ya uvuvi na badala yake akaishi maisha matakatifu ambayo alikuwa amejitolea kwa utumishi wa Mungu.

Habari njema za injili ni kwamba Mungu yu tarari kukupatia kipawa cha Roho Mtakatifu ili kukuwezesha kuishi maisha yenye nguvu sisizoisha na ya utakatifu.

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)

MAMBO AMBAYO

BIBLIA

Inafundisha Kuhusu...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, I Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

I Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, I Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, I Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

Mwanadamu hawesi kuishi maisha ya utakatifu kwa nguvu au uwezo wake mwenyewe. Yesu alikuwa msalabani ili dhambi zetu zipate kusamehewa kupitia kwa utakaso wa damu yake. Tunapotubu tunafanywa chombo safi kupitia Yesu Kristo. Lakini tusikome hapo tu pa kuwa chombo safi. Yesu alikuja ili tupate kujazwa na Roho Mtakatifu. Kama mtu hamtafuti Mungu baada tu ya kuokoka ili kupata Roho Mtakatifu ibilisi atajaribu kujaza maisha yake dhambi na uchafu wa dunia. Ni ujazo wa Roho Mtakatifu pekee ndio utawaponya wanaorudi nyuma na kuwawezesha kuishi maisha matakatifu. Yesu alikuja kufanya kazi kamili ya kuwapa watu nguvu za kuishi kwa utiifu na utakatifu kulingana na Neno la Mungu. Alikuja kuondoa dhambi iliyotendwa na kuwabatiza watu kwa Roho Mtakatifu. Ujuzi wa mtu kupata wokovu kamili ni kitu cha ajabu. Jambo hilo linamwezesha mtu kuishi maisha ambayo amejitolea kwa Mungu. Kujazwa Roho Mtakatifu ni ujuzi wa mtu kupata ushindi wakati wa majoribu, maanake uwezo wa kushinda majoribu, na hata kuweza kupata amani wakati wa dhoruba za maisha. Ni jambo ambalo linamletea mtu moto na uhai maishani mwake ya kila siku ya kuishi kama Mkristo. Ujazo wa Roho Mtakatifu ndilo hitaji kubwa sana ambalo watu wanaokiri kuwa Wakristo wanahitaji. Kuna nguvu ndani ya Roho za kumwezesha mtu kuishi bila dhambi hadi hapo Bwana atakaporudi. Je, wewe unao ujuzi wa kupata mpango huo kamili wa wokovu? Je, umempokea Roho Mtakatifu tangu uwe muumini?

—mws

UKWELI WA INJILI

Gazeti la ‘Ukweli wa Injili’ huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaotetwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinasi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

UAGIJAJI

Ukweli wa Injili ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongozwa. Tudembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

The Gospel Truth, PO Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



"Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa." —Yohana 7:38-39

Kiini cha wokovu kamili hupatikana katika kuwepo kwa Roho Mtakatifu maishani mwa mtu. Roho huleta uhai na uchangamfu wa maisha kwa wale ambao wamepata utamu wa uwepo wako. Ni ujuzi wa ajabu Roho Mtakatifu kudumu katika hekalu hili la kidunia.

Katika robo hii ya mwaka *Ukweli wa Injili* inashughulikia swala la "Kujazwa na Roho Mtakatifu." Lakini haikuwa rahisi mimi kuandika kuhusiana na swala hili katika sehemu hii ndogo ya gazeti kwa maana hili ni somo kubwa sana. Kuna mambo mengi ya kimwili na kidunia ambayo yanapatikana kati ya watu wengi wanaojiita watakatifu. Roho Mtakatifu anaweza kusuluhisha matatizo mengi ambayo yanapatikana katika maisha ya watu binafasi, katika ndoa zao, na katika kusanyiko zao za kanisa.

Kipawa hiki cha Mungu kinajulikana kwa majina mengi: kazi ya pili ya neema, kujazwa na Roho Mtakatifu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, utakaso, mtu kufanya kuwa mkamilifu, n.k.

Kumekuwa na hali kubwa ya kuchanganyiwa katika mafundisho kuhusiana na swala hili. Pia kuna migawanyiko mingi na mafarakano ambayo yameingia katika mwili wa Kristo kuhusu swala hili. Lakini kamwe hatustahili kuruhusu mifano au mawazo ya kumpendeza mwanadamu kuongoza viwango vya ukweli, na badala yake tunahitaji kuruhusu Neno la Mungu kuwa ndio mwongozo wetu kwa yale tunayoelewa. Hata ingawa ni muhimu kwetu kuelewa ukweli rahisi na safi wa yale ambayo Maandiko yanatundisha kuhusiana na swala hili, ni muhimu zaidi kwetu kupata ujuzi huo wa kujazwa Roho Mtakatifu.

Lakini somo hili si ngumu na halichanganyishi watu kama ambavyo adui angetaka kutuonyesha. Yesu alizungumza kwa urahisi kabisa kuhusu Roho Mtakatifu ambaye angewaletea watu wake uwezo maishani mwao. Jambo kuu ambalo maandiko yanafundisha kuhusia na swala hili ni kuhusu Mungu kuwapatia waumini kipawa cha kuwapa uwezo, kuwafariji, na kuaongoza. Neno la Mungu linasema wazi wazi kwamba ujazo wa Roho ni jambo linalofuata kazi ya utakaso wa Mungu maishani mwa mtu. Basi kuna hatari ya watu kuunganisha mambo hayo mawili na kufanya kuwa ni kitu kimoja. Lakilni pia kuna hatari ya watu kujaribu kutenganisha ujuzi huo wa aina mbili hivi kwamba watu wakose umuhimu na thamani ya kupokea Roho Mtakatifu mara tu baada ya wao kuhesabiwa haki. Mambo hayo yote mawili yalikuja kupitia kwa kafara na mpango wa Yesu Kristo.

Watu wengi katika siku zetu hawana nguvu na moto wa maisha yao ya kiroho. Mimi mwenyewe naweza kutoa ushuhuda kuhusu nguvu za Roho Mtakatifu ambazo humtakasa Mkristo, kumpa nguvu mpya, kumwezesha, na hata kumfanya kukomaa maishani. Kama wewe hujampokea Roho Mtakatifu huu ndio wakati mwafaka wa kuomba na mwenzako ili wewe nawe upate ujuzi wa kuishi maisha kamili ya kumuishia Mungu kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Michael W. Smith

April 2014

mengi kwa
MTANDAO

Tutembelee kwa

www.thegospeltruth.org

ili uagize na kusoma

jarida letu.



Wakati wa Kumtafuta Roho Mtakatifu

Wakristo wengi hukawia kutafuta ujazo wa Roho Mtakatifu. Wao hukawia sana hivi kwamba wanapoteza wokovu wao kwa ukosefu wa nguvu maishani mwao.

Biblia yenye wakati hukawia kutafuta ujazo wa Roho Mtakatifu; lakini kulingana na mifano tunayopata katika Maandiko ni jambo muhimu kwa waokovu wapya kumtafuta Roho Mtakatifu.

Yesu mwenyewe hakutaka wanafunzi wake kukabiliana na ulimwengu bila kuwa na uwezo na ndipo akasema: "Lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu" (Luka 24:49). Mtume Paulo alijazwa Roho Mtakatifu muda kidogo baada ya yeze kuokoka. Wakati watu wa Samaria walipomkubali Kristo mara moja wanafunzi wa Yesu walituma mtu kuwalettea ujumbe kuhusu Roho Mtakatifu.

Kuna hatari kubwa mtu kukawia. Punde tu mtu aliyesabiwa haki anapotambua hitaji lake, huo ni wakati mwafaka wake kujazwa na Roho Mtakatifu.

MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA SOMO: KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU

Somo la Biblia:

Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upopo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu... — Matendo 2:1-4a

Muhstasari: Yesu alikufa ili kuwaokoa watu kutoka kwa dhambi zao na kuwaweza kupata ujizi wa kujazwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu humpatia muumini uwezo wa kuishi maisha matakatifupitia kwa nguvu zake za kiungu, uongozi anaompatia Mkriso, na kupitia kwa faraja yake.

I. Unabii kumhusu Roho Mtakatifu

- A. Yoeli 2:28-29 Mungu atamwaga Roho wake.
- B. Ezekiel 36:26-27 Mungu aweka Roho wake ndani yetu.

II. Ahadi ya Roho Mtakatifu

- A. Mathayo 3:11 Yesu anabatiza na Roho Mtakatifu.
- B. Yohana 14:16 Mungu atatoa.
- C. Luka 24:49 Yesu atatuma.
- D. Matendo 1:4-5 Subiri ahadi yake Mungu.

III. Hekalu la Roho Mtakatifu

- A. Matendo 7:44-49 Hema/hekalu la Agano la Kale.
- B. 1 Wakorintho 3:16-17 Nyinyi ni hekalu la Mungu.

IV. Roho Mtakatifu ni Kipawa kwa Watu Wote

- A. Matendo 2:38-39 Kwenu na kwa ajili ya watoto wenu.
- B. Matendo 10:45 Wayahudi na Watu wa Mataifa.

IV. Matakwa ya Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu

- A. Matendo 2:38 Tubuni.
- B. Matendo 19:2 Kuamini.
- C. Matendo 5:32 Kuti.
- D. Warumi 12:1-2 Kujitoa kwa Mungu.

IV. Roho Mtakatifu Hutolewa kwa Wale Tu Ambao Wamehesabiwa Haki

- A. Matendo 8:5-6, 12-17 Kanisa la Samaria.
- B. Matendo 9:17 Mtume Paulo.
- C. Matendo 10:1-2, 44-47 Nyumba ya Kornelio.
- D. Matendo 19:1-7 Wanafunzi wa huko Efeso.

VII. Kazi za Roho Mtakatifu

- A. Matendo 1:8 Kumpatia Mkristo Nguvu, Kumwezesha.
- B. Warumi 15:16 Kutakasa.
- C. Matendo 15:8-9 Kusafisha.
- D. Yohana 14:26 Kufariji, Kufunza.
- E. Yohana 16:13 Kuongoza.
- F. Waefeso 1:13 Kuweka muhuri.
- G. 2 Wakorintho 3:6 Kutoa uhai.
- H. 1 Wakorintho 12:4-11 Karama za kiroho.
- I. Warumi 5:5 Kuweka upendo moyoni.
- J. Waembrania 2:11 Kuleta umoja.

VIII. Ushahidi wa Roho Mtakatifu

- A. Warumi 8:16 Roho mwenyewe.
- B. Wagalatia 5:22-25 Tunda la Roho.
- C. Warumi 14:17 Ufalme wa Mungu.

Tamati

Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawе akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?

—Luka 11:11-13

KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU

Nakala ya kuandamana na Mafunzo ya Biblia

TOHO MTAKATIFU APEANWA

Katika siku ya Pentekoste Roho Mtakatifu alianguka toka mbinguni (Matendo 2:1-4) na kujaa miyoni mwa waumini 120. Waumini hao walikuwa ndio wa kwanza katika kanisa la Agano Jipya kupata ujuzi wa mpango wa Mungu ambao ulitimizwa kupitia kwa Yesu Kristu. Katika wakati huo wa ibada za kisherehe na kitamaduni ambazo zilijaa historia ilijoja dhambi na kuanguka kwa watu kuhusiana na mambo ya kiroho, Yesu alileta wokovu kwa mwanadamu hapa ulimwenguni ili mwanadamu aweze kuishi maishaa ya ushindi na utakatifu kupitia kwa utakaso wa dhambi na kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

AHADI YA BABA

Huku akitazamia siku ya Pentekoste Mungu alitangaza kusudi lake katika Ezekieli 36:27: "Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda." Toka wakati huo mwanadamu hangefungwa na shauku zake zinazomwelekeza dhambini kwa sababu sasa Mungu angejitoka kupitia kwa Roho wake ili mwanadamu aweze kuishi kwa utakatifu katika ulimwengu uliojaa dhambi. Baadaye Mungu akanena kuhusu siku hiyo aliposema: "Nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili" (Yoeli 2:28).

MAKAO YAKE

Katika Agano la Kale uwepo wa Mungu ulinena na mwanadamu kwanza kabisa katika hema na baadaye katika hekalu. Mijengo hii iliundwa kwa mikono ya wanadamu: "Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanya kwa mikono, kama vile asemavyo nabii...Mbingu ni kiti changu cha enzi Na nchi ni pa kuwekea miguu yangu; Ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana, Au ni mahali gani nitakapostarehe?" (Matendo 7:45-49). Swali hili linajibowi katika 1 Wakorintho 3:16-17: "Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu

anaka ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi." Mungu anaweza tu kudumu mahali patakatifu na ndiposa Roho wake hangedumu katika hekalu hili la kimwili hapa duniani mpaka hapo ambapo lingeondolewa dhambi kupitia kwa Yesu Kristo.

YESU ALIKUJA KWA AJILI YA KUANDAA NJIA YA KUJA KWA ROHO MTAKATIFU

Yohana Mbatizaji alipomwona Yesu na alinena kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu (ambaye angekuja): "Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye . . . awabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto." (Mathayo 3:11). Yesu alikuja kuandaa njia kwa ajili ya kuja kwa Roho Mtakatifu: "Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu." (Luka 24:49). Ahadi ya Baba ilikuwa ikizungumzia kipawa hicho cha Roho Mtakatifu.

AMETOLEWA KWA WATU WOTE

Kipawa hiki cha ajabu cha uwezo kupitia kwa Roho Mtakatifu kilitolewa mara ya kwanza katika siku hiyo ya Pentekoste kwa waumini wa Kiyahudi, lakini ahadi hiyo ilikuwa kwa ajili ya watu wote katika vizazi vijavyo: "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali" (Matendo 2:39). Roho Mtakatifu hakutolewa tu kwa ajili ya Wayahudi bali pia kwa ajili ya watu wa mataifa: "Na wale waliotahiriwa,

walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 10:45). Kiwango cha uovu ulio ulimwenguni hakijalishi, Roho Mtakatifu angalipo kwa ajili ya kuwasaidia waumini. Watu wengine hufikiria kwamba wanaweza kustahili kumpata Roho Mtakatifu, au kwamba wanaweza kuomba kwa nguvu ili mwishowe wapate jibu la

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)



Ahadi ya Baba

*"Lakini mtapokea nguvu,
akiisha kuwajilia juu yenu
Roho Mtakatifu."
Matendo 1:8*

Mungu. Lakini ukweli ni kwamba, hiki ni kipawa ambacho kinatolewa bila malipo mradi mtu ametimiza matakwa ya kukipata.

JINSI YA KUMPOKEA ROHO MTAKATIFU

Je, mtu anastahili kufanya nini ili kumpokea Roho Mtakatifu? "Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38). Roho Mtakatifu ataingia tu kwa mtu ambaye mbeleni ametubu dhambi zake.

Kujazwa kwa Roho Mtakatifu pia ni kazi ya imani na anatolewa kwa wale ambaao wanamwamini Kristo (Matendo 19:2) na wanaishi kwa kumtii Mungu (Matendo 5:32). Kwa jinsi ambavyo Roho Mtakatifu ataujaza tu moyo ulio safi, Yeye pia atabatiza tu maisha ambayo yametolewa kabisa kwa Mungu: "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu ilioyai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndio ibada yenu yenyemana" (Warumi 12:1). Katika Agano la Kale moto ulichoma dhabihu ambazo ziliwekwa madhabahuni, ndivyo navyo Roho Mtakatifu (ambaye pia amepewa mfano wa moto) atawaangukia tu wale ambaao wamejitolea kabisa kwa ajili ya mapenzi na kusudi zake Mungu. Basi wewe unahitaji kutubu, kutii, na kujitolea kwake Mungu ambaye naye atakubatiza kwa Roho wake Mtakatifu.

NI KAZI AINA MBILI TOFAUTI

Kujazwa kwa Roho Mtakatifu ni kazi tofauti na maalumu ambayo ni tofauti na ujuzi wa mtu kuhesabiwa haki. Maandiko ambayo tumetoa hapo mbeleni yanaunga mkono kazi hii ya aina mbili ya wokovu kama vile ambavyo mifano mingine yote ya kanisa la mitume inavyofanya katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Filipo alimhubiri Yesu kwa watu wa mjia wa Samaria. Wengi wao wakampokea Kristo na wakabatizwa. Baadaye Petro na Yohana wakaja Samaria kuwaombea ili "wampokee Roho Mtakatifu" (Matendo 8:15). Mungu akawaokoa kutoka kwa dhambi zao na baadaye akawajaza Roho wake. Naye ndugu Sauli, ambaye jina lake baadaye lilibadilishwa na kuitwa Paulo, alimkubali Kristo na ndipo akampokea Roho Mtakatifu kupitia

Roho Mtakatifu

*humpatia Mkristo nguvu wakati wa udhaifu,
neema wakati wa majaribu,
na ushindi wakati anapopambana
na hali ya udhaifu.*

kwa maombi ya Anania. Hivyo ndivyo pia ilikuwa kwa Wakristo wengine, kama inavyoonekana katika nyumba ya Kornelio (Matendo 10) na kwa wanafunzi wa Efeso (Matendo 19) ambaao walijazwa Roho Mtakatifu wakati tofauti na walipookoka.

ROHO MTAKATIFU HULETA NGUVU ZA USHINDI

Roho Mtakatifu ana kazi nyingi na huleta tofauti kubwa sana katika maisha ya muumini. Kwa maneno ya Kristo mwenyewe Roho Mtakatifu huleta nguvu—nguvu za mtu kuishi akiwa huru kutokana na dhambi, nguvu za kushinda ubinafsi na mwili, nguvu za kuishi maisha matakatifu, na nguvu za mtu kuishi kulingana na neno la Mungu: "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." (Matendo 1:8). Roho Mtakatifu humpatia Mkristo nguvu wakati wa kushindwa, neema wakati wa majaribu, na ushindi wakati anapopambana na hali ya udhaifu. Wenye haki "(h)utakaswa na Roho Mtakatifu" (Warumi 15:16). Wao hutengwa na kutolewa kwa Mungu na kufanya watakatifu kwa nguvu zake Mungu. Miyo yao huoshwa na Roho (Matendo 15:9) na kupidia kwa nguvu zake Roho mielekeo yao ya kawaida ya kimwili inafungwa na badala yake kunakuweko na uwezo wa kiungu wa kusema "la" kwa ibilisi na kusema "ndio" kwa Mungu.

KAZI ZINGINE ZA ROHO MTAKATIFU

Roho Mtakatifu ni mfariji na mwalimu (Yohana 14:26). Yeye huongoza na kuwaonyesha njia watu wa Mungu. Roho Mtakatifu ndiye kiongozi na huwapa watu wa Mungu karama za kiroho

(1 Wakorintho 12:4-11). "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu" (Warumi 5:5). Roho Mtakatifu huleta umoja kati ya watu wa kweli wa Mungu (Waebrania 2:11). Yeye huwapa watu wa Mungu uhai, shauku, na kusudi la maisha. "Andiko huua, bali roho hahuisha" (2 Wakorintho 3:6b). Kunazo sifa, utakatifu, na ibada za kweli katika maisha ya wale ambao wamejazwa Roho Mtakatifu.

USHAHIDI WA ROHO MTAKATIFU

Kujazwa kwa Roho Mtakatifu ni kazi ya imani na haimjii mtu kwa njia ya kujidhihirisha kwa kiwango kikubwa ama kwa hisia kubwa: "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:16). Walimu wengi wa uongo husema kwamba ushahidi wa Roho Mtakatifu ni mtu kunena kwa lugha isiyo na maana, wakisema hii ni lugha ya mbinguni. Lakini Maandiko hufunza kwamba ushahidi kamili wa Roho ni nini: "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria" (Wagalatia 5:22-23). Ushahidi

wa kweli wa Roho Mtakatifu ni uwezo na nguvu za kuishi maisha matakatifu.

MPOKEE ROHO NA UWE MSHINDI

Ukamilifu na utajiri wa Ufalme wa Mungu ni utakatifu, amani, na furaha ambayo huja kupitia kwa Roho Mtakatifu ambaye anadumu ndani yetu (Warumi 14:17). Wakristo wengi huwa na wakati mgumu kuishi kama Wakristo. Roho zao huwa na shauku la kufanya mapenzi ya Mungu lakini miili yao ni dhaifu. Roho Mtakatifu ambaye hudumu ndani yetu ndiye jawabu kwa matatizo mengi yaliyoko maishani mwa Wakristo na hata katika makusanyiko ya Wakristo. Kwa njia ya unyenyekevu na imani mtu anastahili kumwomba Baba, naye Baba yuko tayari kumpatia yeote amwombaye kipawa hicho cha Roho Mtakatifu bila hata kukawia.

—mws

SWALI na JIBU

Swali: Je, mtu akishajazwa Roho Mtakatifu anawekwa huru kutokana na udhaifu na majoribu ya kibinadamu?

Jibu: Hapana. Ikiwa tungali tuko maishani haya tutakuwa na udhaifu na majoribu ya kimwili. Tofauti ni kwamba, mtu akiwa na Roho Mtakatifu anakuwa na nguvu zaidi na uwezo wa kiungu wa kushinda majoribu. Mtume Paulo alisema katika 1 Wakorintho 9:27: "Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa." Tunahitaji kuendelea kufa kwa ubinafsi wetu na kudumisha maisha yetu katika kunyenyekoa mbele zake Mungu. Tukikosa kuendelea kujitoa kwake Bwana

tunaweza poteza wokovu wetu. Katika maisha haya mwanadamu daima ataendelea kuwa na uwezo wa kutenda dhambi kwa sababu ana uwezo wa kuchagua kile atakachofanya. Kabla ya mtu kujazwa Roho Mtakatifu anakuwa



Kukua Katika Neema

akivutiwa na dhambi. Lakini baadaye anaanza kuvutiwa na utakatifu kutokana na nguvu za utakaso wa Roho aliyeo ndani yake.

Kwa njia ya Roho Mtakatifu tunapewa silaha ya kuweza kuendelea katika safari yetu ya kiroho na kukua kwa mambo ya Mungu: "Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo" (2 Petro 3:18).

Daima maishani mwetu kama wanadamu kutakuwa na sehemu ambayo Roho Mtakatifu atakuwa angali akifanya kazi ndani yetu ili tuwe wakamilifu zaidi. Watu ambao wamejazwa Roho Mtakatifu wataendelea kudhihirisha uanadamu wao na maumbile yao, lakini Roho ataendelea kufanya kazi ndani yao ya kuwaunda upya ili wakaribie mfano wake Yesu. Kutakuwa na umoja wa malengo na shauku ya kutimiza mapenzi ya Mungu. Nao watakatifu wa Mungu wanaweza (na kwa kweli wataweza) kuishi maisha matakatifu ambayo hayana dhambi.

Kusema kweli Wakristo wataendelea kutenda makosa ya kibinadamu katika safari hii ya kukua kama Wakristo, lakini moyo wa Mkristo unaweza kudumu akiwa mkamilifu mbele zake Mungu. Lakini kungali kutakuwa na sehemu maishani mwetu ambako Roho ataendelea kufanya kazi yake ili kukuza ndani yetu hali ya kiroho ambayo imekomaa zaidi.

—mws



JE, WAJUA?

Wakati wanafunzi walinena kwa "lughu nyingine" wakati walipojazwa Roho Mtakatifu hawakunena kwa lugha isiyo na maana, na pia hawakunena kwa lugha ya mbinguni. Wao walikuwa wakinena lahaja na lugha za mataifa mengine. Kwa maana "kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe" (Matendo 2:6).



Kipawa hiki cha "kunena kwa lugha nyingine" kilikuwa cha kimuu jiza kwa sababu hapo mbeleni wanafunzi hao hawakuwa wamejifunza lugha waliyokuwa wakizungumza. Jambo hili lilisaidia kueneza injili na kutilia mkazo kwamba wokovu ulikuwa ni kipawa kwa watu wote.



Wasiandamane Naye Tena

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65114
USA
Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Kwa ajili ya hayo wengi mionganini mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena. —Yohana 6:66

Yesu Mwana wa Mungu aliyepakwa mafuta alipitia hali nyingi za kukataliwa na watu akiwa humu duniani katika huduma yake. Sio eti kwamba wengine hawakumpokea, kuna hata wanafunzi ambao wakati mmoja walikuwa wakimfuata na kusikiliza mafundisho yake na ambaa baadaye walimgeuka na kuacha kuandamana naye tena. Toka wakati huo wanafunzi hao wakaacha kujitambulisha naye na pia wakaacha kumtambua kama Masiya.

Wengi wao walichukizwa na ujumbe wa injili. Kwa akili zao za kimwili wao hawakuwa tayari kuchunguza maisha yao kwa kioo cha usafi wa ukweli. Pia hawakuwa tayari kujikana na kumfuata Bwana kwa miyo yao yote. Bila shaka jambo hili liliuumumiza Yesu sana. Yeye aliacha ukuu wake mbinguni na kuja duniani kutoa uhai wake kwa sababu ya upendo wake mkuu.

Kama ilivyokuwa wakati wa Yesu ndivyo ilivyo kwa wahudumu wa kweli wa injili hata katika siku zetu. Kutakuwa na watu ambao watakataa huduma yako, watakana vile wewe umejinyima, watakakana hata upendo wako. Wao watachukizwa na ukweli, na wengine hawatakuwa tena na ushirika na wewe.

Wakati mwingi watu kama hao watamlamu mhudumu huyo ama ushirika wa kanisa lao badala ya wao kukubali kwamba wamekataa kazi ya Mungu maishani mwao. Jambo hili huleta uchungu mwingi na mateso rohoni mwa mchungaji wa Bwana. Lakini wewe mchungaji endelea kuwa mwaminifu na usiache kuhubiri ukweli wa kufanya watu kuchunguza miyo yao eti ndio watu wengi wavutiwe kuja kanisani mwako. Wewe endelea kuhubiri ukweli wote kwa unyenyekevu na kwa upendo. Ukweli ambao unawaleta washirika wako hukumu za haki.

Ndugu Ostis Wilson alikuwa akisema yafuatayo: "Ukipendeza Mungu utawapendeza wote ambao wanastahili kupendezwa."



—mws